**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam**
**Tarehe 22 Septemba 2007**

**Mahudhurio**
Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishehe
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Godfrey Jax (CHABADA and UWABA)
Izdoly Aludo Kihalule
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Kibwana Mohammad Msiga
Patrick Masinga
Paulo Atibu Hatibu
Rahma Ali
Ramadhani Rajabu Nyengo
Selion Elieskia
Sudi Saidi Ramadhan

**Mgeni**
Hussein Ally - CHABADA

**Msafara wa Baiskeli**
Juma na Godfrey Jax walitoa taarifa kuhusu siku ya kimataifa ya Michezo, mazoezi na Afya ambayo ilifanyika mwezi mmoja iliyohusisha vyama mbalimbali vya michezo ikiwemo CHABADA. Juma alihudhuria na kugawa vipeperushi.

Ndani ya wiki hiyo Juma alipeleka barua za kuomba ufadhili kwa CRDB, NMB, ubalozi wa Ireland na DSI bicycles tyres. Atafuatilia Mohamed Enterprises wiki hii.

Ndani ya wiki hii tulipokea barua kutoka Manispaa kuthibitisha matumizi ya Mnzi Mmoja kwa tukio la msafara hata hivyo barua ilitutaka kulipa Tsh 150,000 ingawa Azzan Zungu alisema tungepewa bure. Elaine na Godfrey waliongea na mhusika kwa simu kwa nyakati tofauti na kudai kwamba tuandike barua ya kuomba kutumia Mnazi Mmoja bila malipo (pamoja na ukweli kwamba barua yetu ya awali aliomba hilo). Elaine alisema angeandaa barua. Hawakusema pia kama tutatumia mahema.

Hussein Ally alisema kuwa vipaza sauti vyake bado havijatengenezwa lakini angetoa taarifa wiki ijayo.

Juma alipeleka barua za mwaliko kwa karume saccos, Klabu ya michezo ya walemavu na Askari wa usalama barabarani. Pia alipeleka barua ya shukrani kwa Ultimate Security kwa ofa ya gari la wagonja waliyotoa na ufafanuzi kuhusu tarehe ya tukio.

SUMATRA walijibu barua yetu ya mwaliko kwa kuunga mkono UWABA lakini hawakuwa wazi kama watahudhuria au la.

Elaine alinunua wino wa mashine ya kuchapa kwa pesa za UWABA ili kuchapa tiketi na gharama zingine za uchapaji kama tulivyokubaliana wiki iliyopita. Alitumia pesa ambayo ilichukuliwa benki maalum kwa ajili ya kupiga fotokopi mabango na vipeperushi – pesa nyingi zaidi zitachukuliwa benki kwa ajili ya hili hapo baadae.

**Wakala wa Barabara (TANROADS)**
Juma alipata barua kutoka kwa wakala wa Barabara iliyoeleza kuwa tukutane nao Jumatano tarehe 26 saa 4 asubuhi Elaine alizungusha hotuba ya UWABA kwa TANROADS mkoa wa Dar es Salaam ambayo alichukua kama ilivyo na kuifanyia marekebisho kwa ajili ya TANROADS makao makuu. Wanachama walikuja na mapendekezo ambayo yataambatanishwa .

- Iwekwe bayana ni taasisi gani ya serikali inayohusika na taa za mitaani na miti
- Mafuta katika njia za baiskeli yanayowafanya wapanda baiskeli kushukuka yawekwe miteremko
- Mashimo hatari, mitaro isiyo na daraja au nguzo za vyuma chakavu ambazo ni hatari virekebishwe au viondolewe.
- Baadhi ya barabara hazina njia za watembea miguu na baiskeli bali za magari tu
- Kwenye madaraja kuwe na sehemu maalum za baiskeli
- Kwenye baadhi ya barabara sehemu ya baiskeli ni finyu wakati kuna nafasi ya kutosha kupanua
- Sehemu ya barabara ya Morogoro kutoka Ubungo hadi Mbezi ni nzuri kwa kuwa ni pana na njia inapita nyuma ya vituo vya mabasi
- Mifuniko mingi ya mitaro kwenye barabara ya Morogoro imekwisha vunjika.
- Kwenye barabara ya Morogoro njia ya baiskeli hutumia na magari kukwepa Msongamano (foleni).
- Kati ya Tip Top na makutano taxi huegeshwa kando ya barabara na hivyo kuifanya nusu ya njia kuwa maegesho ya taxi.
- Mafuta yawekwe kati ya Manzese na sinza kupunguza mwendo kasi
- Barabara ya Nyerere ilikuwa nzuri sana kwa baiskeli lakini kutokana na kutokarabatiwa imesababisha baiskeli kutumia barabara ya magari
- Barabara ya Tandale Uzuri ina matuta yanayopunguza mwendo kasi wa magari – ni vema
- Mafuta yawekwe katika barabara ya Uhuru kati ya Buguruni na Ilala ili kupunguza mwendokasi.

Elaine atajumuisha mamba haya katika hotuba.

Ilikubalika kuwa baadhi ya watu watakutana saa 2.30 asubuhi Mabibo pamoja na kwenda TANROADS wakati wengine wataenda moja kwa moja TANROADS saa 3.30 asubuhi.

**Ofisi na Guta**
Ally Saidi Mohammed alimaliza kutengeneza sehemu ya kuwekea majarida kwa ajili ya ofisi.

Juma alikuwa hajachukua pesa kwa ajili ya guta kutoka dereva wa guta – Tshs 21,000 sasa inadaiwa.

**Vitambulisho**
Paulo aliviweka magamba vitambulisho ndani ya wiki na kuvigawa Ealine alileta vitambulisho visivyo na magamba na baadhi ya wanachama walisaini vitambulisho hivyo ambavyo vitawekwa magamba na Paulo wiki ijayo. Wengine waliomba vitambulisho viwe katka mtindo mpya (mwingine).

**Fulana (T-Shirts)**
Mejah asingeweza kuja leo kwenye kikao lakini alituma ujumbe kusema kwamba angechapa fulana za UWABA kutokana na mapendekezo yaliyotolewa na wanachama wiki iliyopita zoezi hili litagharimu Tshs 1500 kwa ajili ya uchapaji na fulana isiyochapwa inakadiriwa kuwa Tsh 2500 wafuatao walijiorodhesha kwa ajili ya fulana – Ally Saidi Mishwehe,Elaine baker, Filbert Mbecha , Izdoly Aludo Kihalule, Juma Ali Salehe Jongo, Jumanne Idd Selemani, Patrick Masinga, Paulo Atibu Hatibu, Rahma Ali Ramadhani Rajabu Nyengo, Selion Elieskia, Sudi Said Ramadhani.
Godfrey alisema kwamba kuna eneo ambalo huuza fulana katika barabara ya Morogoro ambalo analifahamu.